Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN5 6DG

ISBN 1 902059 07 -7
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 16-19

Correspondence Course Lessons 16-19

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIANO NA 16.

BABA NA MWANA

Somo: Isaya 45

"Je wewe waweza kupekua kwa kumtafuta Mungu?" (Ayubu 11:7).

Swali hili liliulizwa maelfu ya miaka iliyopita na mtu aliyeitwa Ayubu. Jibu kwenye swali hili ni lilelile leo kama lilivyokuwa wakati ule - kwakweli hatuwezi!

Hatuwezi kujuwa chochote katika yote kuhusu Muumbaji Mkuu wa vitu vyote, mbali kutoka kile Yeye Mwenyewe anacho tuambia katika Neno Lake, Biblia.

Bado hatuwezi kuwa na tumaini la uzima wa milele ila tumjue Yeye.

Njia tu tunayoweza kujuwa kuhusu Mungu ni kwa kusoma kitabu Chake, Biblia ambayo ametupa sisi. Mungu, Mwenyewe amesema:

> *"Mawazo yangu sio mawazo yenu, kamwe njia zenu sio njia zangu, asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu kuliko nchi, ndivyo njia zangu kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu" (Isaya 55:8,9)*

Mungu ni mmoja

> *"Sikia Ee Israeli: Bwana Mungu wetu ndiye Bwana mmoja: nawe umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote" (Kumbukumbu la Torati 6:4-5).*

Musa aliyasema maneno haya kwa Waisraeli jangwani.

Ujumbe kwamba Mungu ni mmoja umerudiwa tena na tena katika maandiko. Kwa Isaya 45:5

Tunasoma:

> *"Mimi ni Bwana, na hapana mwingine, hapana mwingine zaidi yangu mimi"*

Zaidi ya miaka elfu baadaye, mtume Paulo anatuambia kitu kilekile sisi:

> *".....kuna Mungu mmoja, na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Kristo Yesu" (1Timothi 2:5).*

Na tena, kwa 1 Timotheo 6:15-16 Paulo anamsema Mungu kama

> *".....mbarikiwa na Mwenye nguvu pekee Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana; ambaye pekeyake hapatikani na mauti, anakaa kwenye nuru ambayo hakuna mtu awezaye kuikaribia; ambaye hakuna mtu aliyemuona au anayeweza kumuona: ambaye heshima na uwezo unayeye hata milele. Ameni."*

Huyu Mungu mtakatifu ni Mungu mwenye upendo

Kama Biblia imetuambia sisi uwezo na utakatifu wa Mungu tu, hakika tunge muogopa; lakini ingetuwia vigumu kumpenda. Ball Mungu ametuonyesha kwamba Yeye pia ni mwenye rehema na mwema Mwandishi wa Zaburi anatuambia:

> *"Bwana ni mwenye rehema na fadhili, hukawia kukasirika, ni mwingi wa neema.....Kama baba anavyowahurumia watoto wake, ndivyo Bwana anavyo wahurumia wanaomcha. Maana atujuwa umbile letu; anatukumbuka kuwa sisi ni mavumbi" (Zaburi 103:8,13-14).*

Ni katika rehema Yake na upendo Wake Mungu ametupa Bwana Yesu ili aziondoe dhambi zetu.

Mwana wa Mungu

Tangu mwanzo, Mungu aliazimu kumtuma Mwanawe ili awe Mwokozi wetu. Kuna unabii

mwingi unao muhusu Yesu kwenye Agano la Kale, kama unabii mmoja huu ulio kwa Isaya 7:14, tunasoma:

"Tazama, Bikira atachukuwa mimba, naye atazaa mwana na atamwita jina lake Immanueli."

Immanueli maana yake, 'Mungu, pamoja nasi', na Mungu yupo hapa kutoa ahadi ya kumtuma mwanawe.

Wagalatia 4:4 "Lakini wakati ulipo wadia, Mungu alirntuma Mwanawe ambaye alizaliwa na mwanamke, aliye zaliwa chini ya sheria".	Marko 1:11 "Ilikuja sauti toka mbinguni ikasema, 'Ndiwe Mwanangu. nil iye pendezwa". (Hivi wakati wa ubatizo wa Yesu').	Yohana 20:31 ".....ili muamini ya kuwa Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu; na kwamba kwa kuamini ninyi mpate uzima katika jina lake."

Yesu hakuwahi kuwepo

Wakati uzazi unapotokea, maisha mapya yanaanza kuwapo, Kuzaliwa kwa Yesu hakukuwa kumetengeka. Watu wengine wanaamini kwamba Bwana Yeau Kristo alikuwapo kabla ya kuzaliwa na Mariamu.

Kuna maana ambayo unaweza kusema kwamba Yesu alikuwapo tangu mwanzo, kwasababu Mungu aliazimu tangu mwanzo kuwa na mtoto. Sasa, kama Mungu anakusudia kitu chochote, tunajuwa kwa uhakika kabisa kwamba kitatimizwa. Yesu yupo kwenye kitovu cha makusudi ya Mungu, kwahiyo wakati Mungu alipo waambia waaminifu wake katika Agano la Kale kuhusu mapenzi yake, Aliwaambia kuhusu Kristo.

Kwa njia hiyo hiyo Biblia iasema *"Mwana kondoo aliye chinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia"* (Ufunuo 1318). Hii haina maana kuwa Yesu alichinjwa kabla ya kuumbwa ulimwengu - tukio hilo la kutisha lilitokea mara moja, karibu miaka 2000 iliyopita (angalia Waebrania 9:25-28), wakati Yesu aliposulubiwa. Kwasababu kifo

cha Yesu kipo kwenye kitovu mno cha makusudi ya Mungu, Mwenye enzi anakizungumzia kama tukio la rnuhimu sana kwamba kinawavuta watu wote wa nyakati zote - tangu Agano la Kale. Hivyo kimevuta kila kitu *"tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu".*

Biblia mara nyingi inatumia lugha kama hii ili kueleza kuhusu Bwana Yesu, lakini haina maana kwamba Yeye mwenyewe alikuwepo hai kabla hajazaliwa.

Kristo alikuwapo katika nia ya Mungu kama mtu mwingine na Alimleta katika uhai kwa wakati wake ulio pangwa. Lakini haikuwa mpaka mtoto wa Mariamu alipozaliwa huyo Bwana Yesu akawa ni mtu anayeishi.

Maumbile ya Yesu

Kwasababu Yesu alizaliwa na mwanamke, alikuwa na maumbile kama yetu. Kwa Waebrania-2:17 tunasoma:

"Katika mambo yote ilimpasa afanane na ndugu zake."

Kwa kipindi cha uhai wake duniani Yesu alijaribiwa kwa mambo yote lakini kamwe hakutenda dhambi.

Angalia mafungu haya ya maneno, yote yametoka kwa Waebrania, ambayo yanaonyesha kwamba Yesu alishiriki maumbile yetu alipokuwa anaishi duniani:

Waebrania 4:15 "Kwa maana hatuna Kuhani Mkuu ambaye hawezi kuguswa na udhaifu wetu; bali katika hali zote alijaribiwa kama sisi tunavyojaribiwa, lakini hakute nda dhambi."	Waebrania 2:14 "Basi kwakuwa watoto wanashiriki damu na mwili, na yeye Mwenyewe (Yesu) pia alishiriki yayo hayo ...."

Waebrania 2:9	Waebrania 5:7,8
"Lakini "twamuona Yesu, aliye fanywa mdogo kuliko malaika kwa ajili ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima; ili kwa neema ya Mungu aonje mauti kwa ajili ya kila mmoja."	"Ambaye katika siku za mwili, yeye (Yesu) alimtolea dua na maombi pamoja na kulia sana na machozi kwa Yeye awezaye kumuokoa na mauti, naye alisikiwa kwa vile alikuwa mcha Mungu; ingawa alikuwa Mwana aliji funza utii kwa mambo aliyoteseka."

Kwa kweli, Yesu alikuwa namna hii tu kabla ya kufa na kufufuka. Baada ya ufufuo alipewa mwili wenye utukufu na nguvu usiokufa.

Wazo lililopotoka

Watu wengi wamedharau mafundisho ya Biblia yanayohusu Mungu, na hivyo wameamini kitu kinacho itwa "utatu" Wanatuambia kwamba Mungu ana nafsi tatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, wote waposawa. (Kuhusu Roho Mtakatifu tutapima habari zake katika somo la 20.)

Neno 'Utatu' na fungu la maneno Mungu Mwana' hayajajitokeza kwenye Bibiia, Tayari tumekwisha ona mafundisho ya wazi ya Biblia ya kwamba Mungu ni Mmoja, na kwamba Yesu Kristo ni Mwanawe. Kwa njia hiyo hiyo mtoto mwema yupo chini ya baba yake, hivyo Yesu yupo chini ya Mungu. Kamwe hakudai kuwa sawa na Mungu, bali alimtegemea Baba yake kwa mambo yote. Alisema,

> *"Mwana hawezi kufanya lolote binafsi, bali anachoona Baba anafanya" (Yohana 5:19)*

Ni kweli Yesu aliwahi kusema: "Mimi na Baba tu-umoja" (Yohana 10:30). Alikuwa na maana kwamba yeye na Baba yake waliunganika katika nia na kusadi, na aliomba kwamba kwa njia hiyo hiyo wafuasi wake wawe wamoja (Yohana 17:21).

"Na vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, basi Mwana mwenyewe pia atakuwa chini yake yule aliye muwekea vitu vyote chini yake, ili Mungu awe yote katika wote" (1 Wakorintho 15:28).

Huu mstari unatuambia kwamba, hata mwisho wa utawala wake wa miaka 1,000 duniani, Yesu atakuwa chini ya Baba yake, na Mungu atakuwa yote katika wote.

Imani ya Utatu ilitoka wapi?

Wakristo wa kwanza hawakuamini katika Utatu. Waliamini kile Biblia ilichofundisha kwamba kuna

> *".....Mungu mmoja, na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Kristo Yesu" (1 Timotheo 2:5).*

Wazo lisilo la kweli la Utatu lilitoka wapi?

Halikuwa mpaka zaidi ya miaka 300 baada ya kuzaliwa Yesu Kristo ndipo Wakristo walianza kuamini katika 'Utatu'. Wazo hili msingi wake haukuwa kutoka kwenye Biblia, bali juu ya mawazo ya Wayunani, ambao hawakajua kuhusu Mungu mmoja wa kweli. Kidogo kidogo, kanisa liliingiza jambo la 'Mungu watatu katika mmoja', na walikana ukweli wa Biblia kuwa Mungu ni Mmoja.

Imani ya kweli ya Wakristo wa kwanza

'Imani ya Mitume', ambayo ilitungwa karibu miaka 100 baada ya Yesu kwenda juu mbinguni inashika njia ya imani ya Wakristo wa kwanza. Katika hiyo tunasoma:

> *"Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi; na Yesu Kristo Mwanawe wa pekee Bwana wetu, aliyezaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, toka kwa Bikira Mariamu....."*

Haya ni mafundisho ya kweli ya Biblia (sio kama imani zingine). Ukuu na uwezo wa Mungu upo nje ya kitu chochote tunachoweza kufikiri. Hatuwezi kuelewa sana jinsi Mungu wa milele aliweza kuwa na mtoto aliyezaliwa na Mwanamwali mwenye damu na mwili. Lakini Mungu anatujulisha sisi kuwa ilikuwa hivyo, na tunajuwa kuwa neno lake nila kweli. Yatupasa tukubali kwa imani. Ikiwa tunataka kumpendeza Mungu, inatubidi tukubali anachotuambia pasipo kuongeza mawazo ya watu - mawazo ambayo hayajafundishwa kwenye Biblia.

Muhutasari

1. Kuna Mungu Mmoja.
2. Mungu hana nafsi tatu. Mafundisho ya Utatu siyo ya Biblia.
3. Yesu ni Mwana wa Mungu, alizaliwa na bikira Mariamu. Yeye sio Mungu Mwana.
4. Yesu alikuwa mwanadamu; lakini kwasababu Mungu alikuwa ni Baba yake, alikuwa mbali, mbali kuliko mtu yeyote mwingine.
5. Kuzaliwa kwa Yesu ilikuwa ni muujiza, kwasababu mama yake alikuwa Mwanamwali. Baba yake pekee alikuwa ni Mungu Mwenyezi.

Kama unataka kusoma zaidi kuhusu jambo hili, ambalo ni la muhimu sana, omba kitabu YESU - MUNGU MWANA AU MWANA WA MUNGU? Utapata.

Mafungo mengine ya maneno ya kuangalia

Uwepo wa Yesu kama mtu ulianza alipozaliwa	1 Petro 1:20; Waebrania 9:26
Yesu alikuwa mwanadamu	Matendo 2:22; Wafilipi 2:8; Waebrania 2:9, 14-18
Mungu ni mkuu kuliko Yesu	Efeso 4:6; 1 Korintho 11:3; Yoh. 14:28; Yohana 10:29

Sura za kusoma: Kumbukumbu 6; Mathayo 1:18-25
Jifunze kwa moyo: 1 Timotheo 2:5

"Kuna Mungu mmoja, na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu..."

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIANO NA 17.

MAISHA YA YESU

Somo: Luka 2

> "Na malaika akamwambia usiogope, Mariamu: kwa maana umepata kibali mbele za Mungu. Na tazama utachukuwa mimba na kuzaa mtoto, utamwita jina lake YESU. Atakuwa mkuu, na ataitwa mwana wa aliye Juu: na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha baba yake Daudi: naye ataimiliki nyumba ya Yakobo milele; nao ufalme wakehauta kuwa na mwisho" (Luka

Ujumbe gani malaika alio uleta kwa Bikira Mariamu! Lakini kulikuwa na jambo moja lililo mtatiza. Aliambiwa kwamba mtoto ataitwa 'Yesu', alikuwa awe 'Mwana wa Aliye juu'.

Mariamu alimuuliza malaika, "Itakuwaje?"

Malaika alimwambia kwamba Mungu atatumia uwezo wake, Roho Mtakatifu, ili azaliwe Mwanawe. Hakuna mwanaume aliyehusika. Yesa alikuwa Mwana wa Mungu pekee yake.

Soma habari ya kuzaliwa Yesu katika Mathayo sura 1 na 2, katika Luka 2. Utakuta kwamba hakuna sehemu inayo taja kwenye mafungu haya ya maneno kuwa Yesu alikuwepo mbinguni kabla ya kuzaliwa. Wazo kama hili lingepingana na maelezo ya Biblla ya kutungwa mimba na kuzaliwa.

Kubatizwa Kwa Yesu

Biblia inatuambia kidogo sana kuhusu Yesu akiwa mtoto. Inatupeleka kwa haraka kwenye ubatizo wake uliofanywa na Yohana Mbatizaji kwenye Mto Yordani. Ubatizo huu haukuwa wa kumnyunyizia maji. Ulifanyika kwenye mto, na baadaye alitoka nje ya maji (Mark. 1:10). Mbingu zilifunuka, na Mungu alimtuma Roho wake Mtakatifu kwa Yesu. Kulikuwa na sauti kutoka mbinguni iliyo

sema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, niliyependezwa naye" (Math.3:17).

Mwenyewe allvyobatizwa ubatizo ulivyo wa muhimu, na Mungu aliongeza kibali Chake. Baada ya ubatizo wake, tunasoma kwamba Yesu alikwenda jangwani, ambako "alijaribiwa na ibilisi" (Mathayo 4:1).

Alikuwa wa kweli ibilisi ambaye alimjaribu Yesu?

Nini hasa kweli kilichotokea jangwani? Palikuwa na mwanadamu mwenye uwezo mkubwa? Hebu tutazame kwa makini majaribu mawili kati ya matatu.

> "Na Ibilisi, akamchukuwa hadi kwenye mlima mrefu, akamuonyesha falme zote za ulimwengu kwa kitambo kidogo. Na ibilisi akamwambia, Enzi yote hii nitakupa wewe, na utukufu wake: kwa maana zimo mikononi mwangu; na yeyote nimtakaye nitampa. Kwa hivi kama wewe utanipigia magoti mimi, zote zitakuwa zako" (Luka 4:5-7)

Kulikuwa hakuna mlima mrefu katika eneo alilokuwepo Yesu, au kweli sehemu yoyote ya ulimwengu, kutoka ambako unaweza kuona 'falme za ulimwengu wote kwa muda kitambo'. Hivyo Yesu hakuweza kuchukuliwa kwenye eneo kama hili. Mbaii ya hivi, Biblia inasema kwamba ulimwengu upo katika mamlaka ya Mangu, na sio ibilisi. Kwa mfano, Biblia inasema kwa Daniel 4:32, "Aliye juu hutawala katika falme za wanadamu, na humpa amtakaye." Kwa hiyo tunahitajika kutafakari kwa makini kuhusu maana ya jaribu hili.

Sasa hebu tuangalie jaribu lingine toka kwenye majaribu.

Je ni kweli Bwana Yesu alimfuata huyo muovu mkubwa toka jangwani njia yote hadi. Yerusalemu na kisha kukwea kwenye mnara wa hekalu, ili aseme tu alipofika pale, "Imeandikwa, usimjaribu Bwana Mungu wako"? (Luka 4:12).

"Alimchukuwa hadi Yerusalemu, na akamuweka juu ya mnara wa hekalu, na akamwambia, Kama wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini toka hapa: kwa maana imeandikwa, Atakuangazia malaika wakulinde, na kukuongoza: na mikononi mwao wataku chukua, ili usije ukajikwaa mguu wako kwenye jiwe" (Luka 4:9-11)

Hakika, kama kulikuwa na ibilisi wa kweli, Yesu angelimtambua mara hiyo, na angekuwa hana la kumfanya Yesu.

Ikiwa hatuwezi kuyaelewa haya majaribu kama yalivyo fanyika katika njia hii, ni kwa namna gani tuyaelewe basi?
Yesu alijuwa kwamba alikuwa ni Mwana wa Munga, na kuwa atatawala falme zote za ulimwengu. Aliwaza moyoni hizi falme na utukufu wake katika akili yake alipokuwa jangwani. Lakini Yesu alijuwa pia toka Agano la Kale kwamba ilibidi afe kwanza, kabla ya kuweza kutawala ulimwengu.

Aliweza kuwaza kwamba yeye mwenyewe kujitupa chini toka kwenye hekalu itakuwa njia nzuri yeye mwenyewe kuangalia, na kuthibitisha kuwa alikuwa ni Mwana wa Mungu. Hiyo ingerahisisha kazi yake ya kuhubiri. Lakini hiyo haikuwa ni njia aliyo itaka Mungu iwe. Kwa hiyo tunatoa shauri kwamba majaribu yalifanyika katika akili ya Yesu wakati alipokuwa jangwani. Roho Mtakatifu alipewa mara alipobatizwa. Alikuwa na nguvu kubwa, na ilikuwa nguvu au jaribu kubwa la kuweza kuijaribu hii nguvu, hata kama ilikuwa ni kutengeneza mkate toka kwenye mawe tu.

Lakini Yesu alijuwa kwamba nguvu za Mungu zitumike vema. Kwa kumzungumzia ibilisi Maandiko yanatoa njia yenye nguvu sana katika kuelezea shurutisho la mwili wa mwanadamu, majaribu yanayotoka katika nia zetu zote kufanya maovu. Yesu alikuwa na majaribu kama sisi tulivyo - bali yeye kamwe hakukubaliana nayo.

MWILI WA BINADAMU (kama sisi)	MWILI WA UUNGU (kama Mungu)
Tunazaliwa Tunaweza kujari biwa na kutenda dhambi Tunakufa	Mungu siku zote amekuwapo (Zaburi 90:2) Mungu hawezi kujaribiwa na hawezi kufanya dhambi Mungu hawezi kufa. Kwasababu hana uharibifu.

Yesu alikuwa na umbile gani?

Mungu alikuwa ni Baba wa Yesu, lakini mama yake alikuwa ni Mariamu - mwanadamu. Yesu alikuwa ni Mungu, au mwanadamu kama sisi?
Yesu alikuwa na umbile la kibinadamu

1. Siku zote hakuwepo. Maisha yake yalianza wakati alipozaliwa.
2. Alijaribiwa. (Bali, sio kama sisi, hakutenda dhambi).
3. Alikufa. (Lakini, kwasababu alikuwa hana dhambi, Mungu alimfufua yeye kutoka wafu.)

Ingawa alikuwa Mwana wa Mungu, na alikuwa na Roho Mtakatifu, au nguvu za Mungu, bado alikuwa ni mwanadamu. Kama tulivyoona kwenye somo lililopita, mistari ifuatayo ni wazi inaonyesha hivi: Waebrania 2:9, 14-18; 1 Timotheo 2:5; Matendo 2:22. Hatuwezi kwa kweli kufahamu jinsi alivyo kuwa na Baba Mungu na mama mwanadamu. Tukubali Biblia inavyosema kuhusu Yesu. Biblia inatuambia jinsi alivyo inuliwa na utukufu wake Yesu alionao sasa (soma Wafilipi 2:9-11) na inatubidi tukubali hili pia.

Utumishi wa Yesu
Baada ya ubatizo wake na halafu majaribu jangwani tunasoma kwamba Yeau alisafiri miji yote na vijiji, na kuhubiri habari njema za Ufalme wa Mungu: na wale kumi na mbili pamoja naye.

Sasa hebu tutikiri kuhusu mafundisho yake, miujiza yake, njia aliyo ishi, na njia aliyokabili kifo chake.

1. Kufundisha kuhusu tutakavyo ishi

Sura za 5, 6 na 7 za Mathayo zimejaa mafunzo yenye busara. Sura hizi tatu zimejulikana kama 'Hotuba ya Mlimani'. Tambua kitu cha kwanza alicho sema Yesu: "Heri masikini wa roho: kwamaana ufalme wa mbinguni ni wao" (Mathayo 5:3).

Kwasababu Yesu aliuzungumzia 'ufalme wa mbinguni', watu wanadhani kwamba ufalme upo katika mbingu. Lakini tazama mstari wa tano kwenye sura hii: "Heri wapole: kwa maana watarithi nchi." 'Ufalme wa mbingu' maana yake ni Ufalme wa au ulio wa mbinguni'. Tazama maneno ya maombi ya Bwana, kwa Mathayo 6:10, ambapo Yesu anawaambia wanafunzi jinsi ya kuomba, "Mapenzi yako yafanyike duniani kama yanavyo fanyika mbinguni". Ufalme wa mbinguni utakuwa duniani.

Hapa kuna mambo mengine ambayo yalifundishwa na Yesa kwenye Hotuba ya Mlimani. Aliwaa mbia watu kwamba:

* wawapende adui zao
* wasiwahukumu watu wengine
* kumtazama mwanamke kwa tamaa (pamoja na haja ya kujamiiana) ni vibaya ni sawa na kutenda uzinzi
* nuru yao na iangaze (hiyo ni, kuonyesha imani yao katika maisha yao)
* wakati wa kutoa, ifanyike kwa siri
* wasijali mambo ya maisha haya, wa mwamini Mungu kwa kuwagawia mahitaji yao
* wautafute kwanza Ufalme wa Mungu.

Yesu aliwaonya wao pia - na sisi - kwa Mathayo 7:13-23:

* kwamba wachache wataipata njia iendayo uzimani
* kwamba wengi hawatopata walichotegemea wakati watakapo kuta hawana nafasi katika Ufalme wa Mungu (ingawa walifanya mambo ya ajabu kwa jina lake).

2. Afundisha kwa mifano

Mathayo 13 ina mifano mingi. Utaona kwamba mingi ya hii mifano inahusu Ufalme. Mifano kwa Luka 15 inaonyesha kiasi ambacho Mungu anatutaka kuukana ulimwengu, na •tuutafute Ukweli Wake.

3. Mafunzo kwa unabii

Mathayo 24 ni unabii ambao Yesu aliwapa wafuasi wake ili wajue lini hekalu la Yerusalemu litaharibiwa, kama Yesu alivyosema itatokea (Hii ilitokea mnamo A.D. 70.) Vilevile walitaka kujua ishara ya ujio wa Yesu mara ya pili na mwisho wa ulimwengu. (Hii ime jadiliwa katika Somo la 8, ambalo unaweza kusoma tena). Mafundisho mengi ya Yesu yalihusu Ufalme wa Mungu unaokuja.

Miujiza ya Yesu

1. ***Miujiza ya uponyaji:*** Injili zina matendo ya ajabu ya uponyaji ambao Yesu alifanya. Aliwahurumia watu, na alitaka kuwasaidia. Uwezo wake ulikuwa ni mkubwa hata ali weza kuwafufua waliokufa.
2. ***Miujiza mingine:*** Yesu aliweza kugeaza maji kuwa divai, alitembea baharini, aliwalisha watu maelfu. Siku zote alitumia uwezo wake katika kuwasaidia watu - kamwe si kuwa furahisha watu au 'kuwa koga'. Miujiza ilikawa ni ishara ya uwezo wake na mamlaka, ilitoa nafasi kwa kufundisha na alionyesha wema wake na huruma.

Maisha ya Yesu

Mwana wa Mungu alizaliwa kwenye hori ya kulishia ng'ombe. Mara nyingi alikuwa hana pakuishi. Alisema: "Mbweha wana mashimo, na ndege wana viota; bali Mwana wa Adamu hana pakulaza kichwa chake" (Luka 9:58). Kabla ya kifo, Yesu aliwaosha miguu ya wanafunzi. Mara nyingi kazi hii ilifanywa na mtumishi. Ingawa alikuwa Mwana wa Muumba mkuu wa ulimwengu wote, Yesu hakuishi maisha ya raha. Ametufundisha na sisi kuwa wanyenyekevu na wenye kuwasaidia wengine.

Bwana Yesu alitumia muda mwingi kwa maombi kwa Baba yake aliye mbinguni. KabIa ya kuwachagua wafuasi wake aliutumia usiku wote katika maombi. Hakuomba mahali palipo wazi, ili ajionyeshe alivyokuwa mzuri. Aliwalauma viongozi wa dini katika njia hii. Alilaumu unafiki wao, na aliwaaabia wao hivyo. Kamwe hakuogopa kutokuwa na watu wenu weng Matayarisho kwa kifo.

Mara (Luka 9:27-36) moja Yesu aliwachukua wafuasi wake watatu hadi mlimani. Na pale alipo omba alibadilika. Musa na Elia walitokea kwake, na walizungumzia kuhusu kifo cha Yesu kilicho kuwa kina mjia Yerusalemu. Maono ya Yesu katika utukufu ilkuwa ni picha yake kwenye ufalme, na ilibidi imsaidie kutazama mbele kwenye ufalme hao, kama alivyokuwa amekiona kifo chake kilichokawa kinakuja.
Alijuwa kutoka Agano la Kale katika unabii yakuwa atakufa kifo cha kikatili. (Zaburi 22 na 69, na Isaya 53 ni baadhi ya unabii wa kifo chake.) Yesu aliwaonya wafuasi wake kuwa atateseka na kuuwawa, lakini aljiwaambia pia kwamba atafufuka toka wafu (Luka 9:22).
Viongozi wa dini walitafuta siku zote kumkamata, na Yesu alijua wanamchukia. Walijaribu mara mbili kumpiga mawe, lakini "saa yake ilikuwa bado kufika". Ulikuwa bado muda wake wa kufa. Lakini-

"Muda ulipowadia ili apokelewe juu, aliukaza uso wake kuelekea Yerusalemu" (Luka 9:51).

Hakuogopa kufa. Alijuwa kuwa ilikuwa ni njia pekee ya kuwaokoa wenye dhambi. Lakini aweza kuwasaidia tu kwa njia hii kama yeye mwenyewe hana dhambi, siku zote alipigana na dhambi - na alishinda! Alituachia sisi mfano wa ajabu.

Na aliwaambia wafuasi wake kwamba wamfuate yeye:

"Kama mtu akitaka kunifoata, ajikane mwenyewe, auchukue maalaba siku zote, kisha anifuate" (Luka 9:33).

Sura za kusoma: Mathayo 5,6 na 7; Luka 9
Jifunze kwa moyo: Luka 1:32

"Atakuwa mkuu, na ataitwa mwana wa wa Aliyejuu: na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha baba yake Daudi"

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIANO NA 18.

KIFO CHA YESU
Somo: Marko 14 na 15
Tatizo la dhambi

Ni wazi kwamba dhambi ni tatizo la kuogofya kwa mwanadamu. Ni tatizo ambalo hata mwanaume au mwanamke mnyoofu mno kamwe hajaweza kulitatua. Haiwezekani kwa mtu kuishinda dhambi kwa juhudi zake mwenyewe. Biblia yote ni kuhuau jinsi Mungu alivyo toa jibu la dhambi za mwanadamu. Mungu alimtoa Mwanawe, Bwana Yesu Kristo awe sadaka ambayo inakubalika kuvunja kinacho shikilia dhambi kwa mwanadamu.

Bwana Yesu aliungana na Baba yake katika kazi hii. Alitoa sadaka yake mwenyewe ya hiari na utii ili kuishinda nguvu ya dhambi juu ya wanadamu na kurahisisha kwa wafuasi wake wa nyakati zote kufanya yale yale kwa kumfuata yeye.

Sadaka ya Bwana Yesu inarahisisha kwa wote wawili Bwana Yesu Kristo na wafuasi wake wote wa kweli kuepuka matokeo ya hukumu ya kifo kilichorithiwa kutoka kwa Adamu. Na vilevile inawezesha kwa wafuasi wa Yesu kusamehewa dhambi zao. (Kwa kweli Yesu alikuwa kamili hakutenda dhambi yoyote).

Unabii wa mateso ya Bwana Yesu Kristo
Tunaweza kusoma kuhusu mateso ya Bwana katika Injili. Lakini tuna picha kamili kama tukisoma baadhi ya unabii vilevile.

Geukia kwa Zaburi 22. Zaburi hii inatusaidia kuelewa jinsi Yesu alivyo jiona wakati wa kusulubiwa:

"Lakini mimi ni mdudu wala sio mtu; laumu ya wanadamu, na dharau ya watu. Wote wanionao hunicheka kwa kubeza: hunifyonya, wakitikisa vichwa vyao, husema, Alimtegemea Bwana kuwa atamuokoa: acha amuokoe, maana alipendezwa naye" (mistari 6-8).

Sio uchungu tu, bali pia aibu ya kusulubiwa uzito ulilemea juu ya Yesu. Soma kwa makini Zaburi hii. Pengine zaidi kuliko maneno mengine yoyote katika Biblia, haya yanatusaidia sisi kufahamu kile ambacho Bwana alikipitia kwa ajili yetu. Tazama tena mistari 15-16:

> "Nguvu zangu zimekauka kama gae; na ulimi wangu waambatana na taya zangu; na umeniweka katika mavumbi ya mauti. Kwa maana mbwa wamenizunguka: kusanyiko la watu waovu wamenisonga: wamenichoma mikono yangu na migau yangu."

Jinsi kifo kilivyo kuja
Viongozi wa Wayahudi walimchukia Yesu. Wakati kusanyiko kubwa lilipokuja kumsikiliza, na walipoleta wagonjwa aliwaponya, walikuwa na wivu na hasira. Hawakuweza kuona kwamba miujiza alio ifanya ilikuwa ni ushahidi kwamba hakika alikuwa ni Mwana wa Mungu. Walipofushwa na chuki na wivu wao. Wakaamua kuwa Yesu inabidi auawe. Walimuhukumu kuwa alikuwa anakufuru, na kukufuru adhabu yake ni kifo kufuatana na sheria ambazo walipewa na Mungu.

Kwa kweli yalikuwa ni mashitaka ya uongo, lakini hawakujali kuhusu hilo! Israeli kwa wakati ule ilitawaliwa na Warumi, na ingawa wakuu wa Wayahudi — makuhani na Mafarisayo - walimuhukumu Yesu kifo, hawakuweza kumuua pasipo ukubali wa Mtawala wa Kirumi.

Jina la Mtawala wa Kirumi wakati ule alikuwa ni Pontio Pilato. Wayahudi walimleta Yesu kwa Pilato na walidai kwamb asulubiwe. Pilato alijuwa vema sana kuwa Yesu alikuwa hana kosa. Alijuwa - kwamba Wayahudi walitaka auawe kwasababu walimuonea wivu Lakini aliogopa kwamba ikiwa akisimama kinyume na Wayahudi, wangepeleka habari kwa Kaisari, na angepoteza nafasi yake. Hivyo kwa unyonge alikubali. Akamkabidhi Yesu ili asulubiwe —hakika kifo cha uchungu na maumivu makali sana walicho vumbua - ingawa alijuwa alikuwa hana kosa.

Kwa hivi Warumi walikuwa pia walaumiwe kwa kile kilichotokea kwa Bwana Yesu.

Kwa nini Yesu ilibidi apate maumivu mno?
Kama tunamfikiria Yesu akiwa ametundikwa msalabani, na kukumbuka kwamba kamwe hakufanya lolote baya, bali siku zote alifanya mambo yale yaliyompendeza Mungu, tunajiuliza wenyewe: "Kwa nini haya ilibidi yatokee kwa Yesu?"

Jambo moja ni hakika; ilikuwa ni njia pekee ambayo wanadamu waweza kuokolewa toka dhambi. Yesu aliomba mara tatu kwa Baba yake, "Kama ikiwezekana, kikombe kiniepake" (Mathayo 26:39). (Ingawa alikuwa makini kuongeza, "Walakini sio mapenzi yangu, bali mapenzi yako, yafanyike" -Luka 22:42.) Kama ingeliwezekana, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu angemuhurumia Mwanawe kwenye uchungu.

Lakini ilikuwa ni njia pekee.

Kwa nini Yesu ilibidi afe?

Adamu alifanya dhambi; kwa hivi Adamu alikufa. Kifo kilikuwa ni adhabu yake. Tunaambiwa: "Mshahara wa dhambi ni mauti" (Rumi 6:23). Hii ni sheria ya Mangu, nayo haiwezi kuvunjika.

Watu wote (isipokuwa Yesu) wanakufa kwasababu: 1. Sole tuna umbo la Adamu linalo kufa; 2. Sisi sote tuna dhambi.	Yesu alikufa kwasababu: 1. Alikuwa na umbo la Adamu linalo kufa; Lakini HAKU tenda dhainbi.
Sababu 2	Sababu 1 tu

Yesu alijaribiwa kama sisi tunavyojaribiwa, na katika njia zingine zaidi yetu, kamwe hakutenda dhambi. Katika Waebrania 4:15 tunasoma:

> *"Yesu katika hali zote alijaribiwa kama sisi, hakufanya dhambi,"*

Kwa hiyo Yesu ilibid**i afe** kwasababu alikuwa na umbile la mwanadamu, lakini hakustahli kufa kwasababu hakufanya dhambi. Kwasababu hii Mungu aliweza kumfufua Yesu toka wafu pasipo kuvunja sheria zake Mwenyewe ambazo "mshahara wa dhambi ni mauti".

Baada ya ufufuo wake Mungu alimpa Yesu umbile jipya— umbile ambalo halifi tena kwasababu ya dhambi ya Adamu na pia umbo ambalo haliwezi tena kujaribiwa kufanya dhambi.

Tunaweza dhambi zetu kusamehewa kwa kuunganika na sadaka ya Yesu katika ubatizo kwa kukiri na kutubu. Wakati Yesu akirudi tena tutaweza pia kushinda kito.

Masomo ya msalaba

Kusulubiwa kwa Yesu ilikuwa ni tukio la kutisha. Ilionyesha ubaya zaidi wa wanadamu kama walivyo mchukua Mwana wa Mungu mkamilifu na mwema aliyependwa na walimuua kwa ukatili. Kumsulubisha kulionyesha jinsi kweli watu walivyo waovo na jinsi wasivyo weza kamwe kujiokoa wenyewe.

Inatubidi tutambue kwamba sisi ni wenye dhambi pia, na tunahitaji mno wokova. Tunafanya vema kufikiria kuhusu ukweli kwamba Bwana Yesu alikuwa ni sadaka inayokubalika. Alikuwa kama mwana kondoo asie na waa na Mungu alikuwa anaikubali sadaka hii kamili kama matoleo kwa ajili ya wote wanao mwamini Yesu kama "Mwana kondoo wa Mungu, achukuae dhambi za ulimwengu" (Yohana 1:29).

Somo lingine la muhimu ni hili: msalaba wa Kristo unaonyesha urefu wa upendo wa Mungu kwetu. Paulo anauweka namna hii:

> "Yeyahakumwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" (Warumi 8:32).

Ni moja pamoja na Mungu

Mwanadamu alitengana na Mungu sababu ya dhambi. Kutengeneza mgawanyo huo umeitwa katika Maandiko

"Upatanisho". Kama ukitazama neno lenyewe utaona linamaanisha nini:

Kupata-nishwa

Hivyo ndivyo dhabihu ya Bwana Yeau inaweza kufanya kwa ajili yetu. Mwishowe itatufanya kuwa pamoja na Mungu; kwa mapatano kamili na makubaliano. Tunaweza kufika kwenye hali hii tukiepuka toka kwa Adamu na kwenda kwa Kristo na tukiwa dhambi zetu tumesamehewa. Kama Daudi anavyosema kwenye Zaburi:

> "Heri aliyesamehewa makosa yake, ambaye dhambi zake zimefunikwa. Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii makosa yake" (Zaburi 32:1,2).

Ni vipi kuhusu upande wetu?

Mungu amefanya yote kwa ajili yetu Ametupa Yesu kama sadaka. Yesu alitoa uhai wake kwa ajili yetu. Lakini kweli tusipo amini kile Mungu alichotutendea, dhabihu ya Yesu haita tufanyia kitu chochote chema.

Tufanye nini? Baadhi ya Wayahudi walimuuliza Mtume Petro swali hili na jibu lake ni haki la kweli kwetu sisi leo. Petro aliwaambia:

> *"Tubuni, na mbatizwe kila mmojawenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi" (Matendo 2:38).*

Tena, kwenye sura inayofuata (Matendo 3:19) mtume anasema:

> *"Kwa hivyo tubuni na mbadilike (mrejee), zipate kufutwa dhambi zenu".*

Neema ya Mungu na imani yetu

Hivyo tunakuja kwenye kitovu cha Injili. Katika utimilifu wa pendo lake, Mungu amemtoa Yesu kwa ajili ya dhambi. Huu upendo wa bure mara nyingi umezungumziwa katika Agano Jipya kama 'neema Yake'. Hivyo kwa Efeso 1:6-8 tunaisoma neema hiyo:

> *"....ambayo yeye (Mungu) ametufanya sisi tukubalike katika huyo mpendwa (Yesu Kristo). Katika yeye huyo tunao ukombozi kwa damu yake, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake; ambayo ametuzidishia sisi katika hekima yote na busara."*

Tunaweza kutupilia mbali neema ya Mungu na upendo. Tunaweza kuudharau. Lakini kama tuna busara, hatuwezi kufanya kati ya mambo haya. Ni mfano mmoja wa ajabu wa toleo la uzima na upendo. Tutahitaji kuwa miongoni mwa wale ambao Yesu anawasema katika Marko 16:16:

> *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka"*

Ubatizo ni mwanzo wa maisha mapya

Sisi ni wana wa Adamu, na kama Adamu, tunapenda njia zetu wenyewe mbali ya njia za Mungu. Lakini Yesu, alipotoa uhai wake kama dhabihu kwa dhambi, amefanya iwezekane kwa ajili yetu kuwa wana wa Mungu na kuwa sehemu ya familia ya Kristo.

> *"Kama mtu akitaka kunifuata, ajikane mwenyewe, na auchukue msalaba wake siku zote, kisha anifuate" (Luka 9:23).*

Yatupasa tubatizwe kufuatana na agizo lake. Hii ina maana kwamba badala ya kutembea katika njia zetu za dhambi, inatubidi tuifie dhambi (yaani, tufanye kila bidii ya kuacha kuendelea kufanya dhambi), na kutembea na Kristo katika upya wa uzima, siku zote

sisi wenyewe tupendelee njia ya Mungu. Mtume Paulo anatuambia sisi:

> "Walio wa Kristo wameusulubisha mwili pamoja na mawazo mabaya na tamaa zake. Kama tukiishi katika Roho, basi tutembee katika Roho" (Wagalatia 5:24,25).

Muhutasari

1. Watu wote wanastahili kufa, kwa kuwa ni wenye dhambi.
2. Mungu kwa upendo wake kwa wanadamu ametoa njia, katika hiyo dhambi zinaweza kusamehewa.
3. Njia hii ni katika kifo cha Mwana wake pekee Yesu Kristo, aliye ishi maisha yasio na dhambi.
4. Ingawa Yesu aliishi maisha yasio na dhambi, alishiriki katika umbile letu ambalo linabidi life.
5. Mungu alimfufua Yesu toka wafu, kwa sababa alikuwa hana dhambi.
6. Kama tunakiri kwamba sisi ni wenye dhambi na tunastahili kufa, na tukija kwa Mungu kwa njia ya Yesu, atatusamehe dhambi zetu.
7. Kama tukiungama dhambi zetu na kubatizwa, tutaweza kuwa wana wa Mungu, pamoja na tumaini la uzima wa milele.

Sura sa kusoma: 2 Wakorintho 5; 1 Petro 1
Mstari wa kujifunza: Warumi 5:8

> *"Lakini Mungu ameonyesha pendo lake kwetu sisi, katika huo, wakati tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu."*

KIFO CHA YESU
Somo: Yohana 20

Kwa huzuni wanawake walikwenda mahali ambako waluona mwili wa Yesu umelazwa. Walichukua manukato ya kuupaka mwili wake. Hawakajua ni jinsi gani watakwenda kuliondoa jiwe kubwa kwenye mwingilio wa kaburi, lakini waliona iliwabidi kwenda na kuupaka mwili wa Bwana wao. Lakini walipofika kaburini —

* jiwe lilikuwa limevingirishwa!

* kaburi lilikuwa wazi!

* na malaika walikuwepo pale!



"Mnatafuta nini kwa wafu?" malaika waliuliza. *"Hayupo hapa amefufuka" (Luka 24:5-6).*

Wanawake walirudi na waliwaambia wanafunzi kwamba Yesu ya hai, bali hakuna hata mmoja aliwaamini kweli. Petro na Yohana walikimbilia Kuelekea kaburini wajionee wenyewe. Hakika kaburi lilikuwa wazi — na sanda za Yesu zilikuwa zimelala pale.

Mariamu Magdalene, mmoja wa wale wanawake, alirudi kaburini, naye kule alilia. Alidhani kuna mtu ameuiba mwili wa Yesu, ingawa malaika walisema alifufuka kutoka wafu Yesu akaja na akazungumza naye, lakini alidhani ni mtunza bustani (Yohana 20:14-18).

KishaYesu akasema, "Mariamu!"

Alitamka jina lake, na mara akajua ni Yesu. Kweli alikuwa pale! Alikuwa hai!

Ni kweli Yesu alifufuka kutoka wafu?
Watu wengi hawaya amini maelezo ya Biblia jinsi Yesu alivyo fufuka toka wafu. Hapa kuna sababu baadhi wanazo toa za kutoamini ufufuo.

1. Wanasema: Yesu hakufa msalabani. Ilionekana tu kama alikuwa amekufa. Uhai wake ulirudi baadaye ndani ya utulivu wa kaburi.
   Lakini - ni wazi Biblia inasema Yesu alikufa msalabani (Yohana 19:33). Katika Marko 15:42-45 tunasoma jinsi Pilato alivyataka kujuwa kama kweli Yesu alikuwa amekufa. Alimtuma askari wa Kirumi kuangalia, naye askari alitoa taarifa kwamba kweli kabisa alikuwa amekufa. Maaskari waliwezakuaminiwa kuona kama mtu alikuwa amekufa au yu hai.

2. Wanasema: "Wanafunzi wake waliuiba mwili."
   Lakini - hii sio kweli. Makuhani wakuu na wazee hawakutaka watu wajue kwamba kaburi lilikuwa wazi, na kwamba Yesu yuko hai tena. Waliwapa pesa watu waliokuwa wanalinda kaburi ili waseme kwamba wanafunzi wake waliuiba mwili. Soma Mathayo 28:11-15, na utaona jinsi uongo huu ulivyo anza.

   Hakuna maelezo katika Biblia yanayoleta hoja kwamba wanafunzi waliuiba mwili. Wanafunzi hawakuamini kuwa Yesu yupo hai mpaka hasa kweli walipo muona. Baada ya kifo chake, wanafunzi waliogopa, wakawa hawana furaha na kutokuamini. Hawakuwa kwenye nia ya kuwadanganya viongozi wa Wayahudi.

   Baadaye, wakati walikuwa na uhakika kuwa Yesu amefufuka, wakawa ni watu waliobadilika. Walihatarisha maisha yao kwa kuhubiri kuhusu ufufuo. Hata baadhi walikufa kwa ajili ya imani yao. Kama kweli waliuiba mwili, na walifanya ujanja huu, wasinge fanya vitu kama hivi.

3. Wanasema: Aliuacha mwili wake nyuma, na akarudi kama roho.
   Lakini -Yesu alifufuka akiwa na mwili. Hakurudi akiwa kama roho. Kama tayari tulivyo kwisha kuona, kweli watu wengi walimuona Yesu. Tomaso aliona mashimo mikononi mwa Yesu na ubavuni; na Yesu alimwambia ayaguse (Yohana 20:27).

   Yesu aliomba chakula, na akala mbele ya wanafunzi wake (Luka 24:41-43). Yesu aliwaambia wafuasi wake: "Nishikeni na muone; kwa maana roho haina mwili na mifupa, kama munavyo niona mimi ninayo" (Luka 24:39).

4. Wanasema: "Wanafunzi walikwenda kwenye kaburi lisilo lenyewe."
   Lakini Biblia inatuambia wazi, katika Marko 16:6, kwamba wanawake walikwenda kaburini ambako mwili wa Yesu ulikuwa umelazwa, na kule malaika walizungumza nao. Iwapo kweli Yesu aliwatokea wanafunzi wake na aliwaonyesha mashimo ya mikono yake, miguu na ubavu, basi inabidi awe ametoka kwa wafu, na kaburi ambamo alikuwa amelazwa ilibidi liwe wazi.
   Na hapana shaka wakuu wa Wayahudi walilipata kaburi lililo sahihi na wangeonyeshwa angali amekufa —lakini hawakuweza, kwa sababu alikuwa yu hai.

Inahitajika imani kukubali kwamba Yesu alifufuka kutoka wafu. Hata mwanafunzi Tomaso hakuamini kwa mara ya kwanza. Hakuamini mpaka alipo muona Yesu mwenyewe. Yesu alimwambia:

"Heri wale ambao hawajaona, na bado wanaamini" (Yohana 20:29).

Wakati wa Ufalme wa Mungu ulikuja?

Mwlsho wakati wafuasi walipotambua kwamba Yesu kweli yupo hai tena, walitumaini kuwa angeweka Ufalme wa Mungu wakati uleule. Maana Bwana alikuwa nao kwa muda wa siku arobaini, akiwafundisha kuhusu Ufalme huo (Matendo 1:3). Ndipo walimuuIiza:

"Bwana, kwa wakati huu utawarudishia Ufalme kwa leraeli?" (Matendo 1:6).

Yesu alijibu:

"Sio kazi yenu kujua nyakati au majira, ambayo Baba ameyaweka katika uwezo wake mwenyewe" (Matendo 1:7).

Kulikuwa na kazi ya kufanya kabla ya kuusimamisha Ufalme. Wafuasi iliwabidi waende ulimwenguni kuhubiri Injili ya Ufalme. Yote haya yalitokea karibu miaka 2000 iliyopita lakini kazi ya kuhubiri bado inaendelea leo.

Kupaa

Wakati Yesu alikuwa anazungumza na wafuasi wake kuhusu mambo haya kwenye mlima wa Mizeituni, nje kidogo ya Yerusalemu, alitwaliwa kutoka kwao kwenda mbinguni. Kama walivyo muona akienda, malaika wawili waliwaambia. Maneno ya malaika yanatuambia wazi kwamba Yesu atarudi.

"Na wakati wamekaza macho kuelekea mbinguni, tazama watu wawili wali simama karibu yao wakiwa na mavazi meupe; kwanini mmesimama mnatazama juu mbinguni? Huyy Yesu yuleyule aliye twaliwa kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja vilevile kama mlivyo muona akienda mbinguni" (Matendo 1:10-11)

Tambua jinsi mstari huu ulivyo dhahiri. Hausemi, "Yesu atarudi tena". Unasema Huya Yesu yuleyule - na kama kungekuwa na shaka yoyote, unasema Huyu Yesu yuleyule aliyetwaliwa toka kwenu kwenda mbinguni.

Walimuona Yesu akienda mbinguni katika mwili (kumbuka hakuwa roho).

Itakuwa ni Yesu yuleyule, na atarudi tena katika njia ileile kama alivyo kwenda. Ilikuwa ni ujumbe wa ajabu ulio na tumaini ambalo wafuasi wa Yesa walipewa na malaika. Yesu atarudi tena, katika umbile la mwili, wakati huu sio kufa, bali kutawala akiwa Mfalme wa dunia yote. Ndipo ataurudisha Ufalme kwa Israel (Matendo 1:6).

Ufufuo wa Yesu — na utufuo wetu

Kwa 1 Wakorintho 15 mtume Paulo anazungumzia kuhusu ufufuo wa Yesu Kristo. Anasema kwamba kama Kristo haku fufuliwa toka wafu, basi Imani yetu ni bure, na dhambi zetu hazija samehewa. Wale ambao wamekufa wamepotea pasipo tumaini (1 Wakorintho 15:17-19). Ni picha gani yenye huzuni!

Lakini, anasema

"Bali sasa Kristo amefufuka kutoka wafu, na amekuwa limbuko (wa kwanza) lao walio lala. Kwa maana mauti yaliletwa na mtu, hali kadhalika kiama ya wafu pia ililetwa na mtu. Kwakuwa kama katika Adamu wote hufa, hata hivyo katika Kristo wata huishwa. Lakini kila mmoja katika utaratibu wake mwenye: Kristo limbuko; baadaye walio wa-Kristo atakapokuja." 1 Wakorintho 15:20-23	Kristo amefufuka kutoka wafu. Yeye ni wa kwanza: wengine watafuata. Mauti yalikuja kwasababu ya Adamu. Ufufuo wa kutoka wafu unaweza kuja tu kwa sababa ya Yesu. Kila mmoja anakufa, kwa sababu kila mmoja yumo "katika mwili wa Adamu". Wote wale walio katika "Kristo" (wanao muhusu Kristo) watahuishwa wakati atakapo rudi katika dunia hii.

Hii ina maana kwamba, kama tunakufa kabla Yesu hajaja, nasi pia tutaweza kufufuliwa kutoka wafu. Tukiwa tu "katika Kristo" ndipo tutapewa nafasi kwenye Ufalme wa Mungu. Tunaweza kuwapo tu kwa haki ya Kristo kama tukibatizwa katika mauti yake (angalia Wagalatia 3:27-29).

Jinsi gani wafu watafufuliwa, na kwa mwili upi watatoka?

Watu walitaka kujua namna hiyo wakati wa Paulo (1 Wakorintho 15:35). Kiasi kama Yesu alivyokuwa na mwili wakati alipo fufuka kutoka wafu, hivyo wale ambao watafufuliwa kutoka wafu atakapo rudi watakuwa na miili-kamwe hawata kuwa roho. Leo Yesu yu haiamepewa mwili usio kufa kamwe.

Ni wazi kabisa, kama unaona wakati ukisoma 1 Wakorintho 15, kwamba wale ambao watapewa uzima wa milele watakuwa na miili itakayo badilika.

Miili yetu ya sasa ipo chini ya mauti, na tunapata uchungu, wakati mwingine tunaugua. Wale watakao pewa nafasi kwenye Ufalme wa Mungu watakuwa na mwili mpya, miili isiyo kufa. Watakuwa hawafi, kama tunasoma 1 Wakorintho 15:50-57.

Ni ofa ya namna gani iliyo ya ajabu tuliopewa na Mungu!

- Tunaweza kupata msamaha wa dhambi zetu kupitia Bwana Yesu.
- Tunaweza kufufuka kutoka wafu kama yeye alivyo fanya.
- Tunaweza kupewa miili isio kufa;
- Tutaweza kupata nafasi katika Ufalme duniani.

Sio ajabu rntume Paulo anasema:

> *"Ashukuriwe Mungu atupaye ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo"*
> *(1 Wakorintho 15:57).*

Ni ujumbe mkuu wa wakovu, Yesu aliwaambia wanafunzi wake wauhubiri ujumbe kwa watu wote. Nasi pia tunahitajika kuupitisha huu njumbe.

Maelezo kwa ufupi

1. Yesu alifufuka kutoka wafu.
2. Hakuwa roho alipofufuka; alikuwa na mwili wa nyama na mifupa.
3. Yesu yu hai leo. Alipaa kwenda mbinguni, aliko sasa.
4. Atarudi duniani kwa njia ileile kama alivyo kwenda mbinguni.
5. Ikiwa sisi ni wa-Kristo, tutaweza kufufuliwa kutoka wafu na kupewa kutokufa miili isiokufa wakati Bwana atakapo rudi.

Sura za kusoma: Matendo 1
Soma pia habari za ufufuo katika Mathayo 28 na Luka 24

Mstari wa kujifunza: Matendo 2:24

> *"Ambaye(Yesu) Mungu amemfufua, akisha kuulegeza uchungu wa mauti: kwasababu haikuwezekana ashikwe nayo."*

MASWALI KARATASI YA 4

Jaribu ujibu maswali kwa jinsi ulivyoelewa. Panaposema "kazi ya ziada" unaweza kujibu swali au ikiwa ni gumu unaweza kuacha. Tafadhali jaribu kujibu maswali yote mengine.

Kumbuka kuweka jina lako kwenye kila karatasi ya maswali na namba yako ya kuletewa masomo.

MASOMO 16-19

16A Kweli au sio kweli? Tenga haya yafuatayo yapi yaliyo sahihi na yasiyo sahihi:

(a) Mama yake Yesu alikuwa Mariamu.
(b) Baba yake Yesu aliitwa Yusufu.
(c) Yesu alikuwepo mbinguni kabla ya kuzaliwa.
(d) Mungu alijua tangu mwanzo ya kwamba angemtuma Yesu.
(e) Yesu alikuwa na umbo la mwanadamu kama sisi alipokuwepo duniani.
(f) Yesu ameitwa "Mungu Mwana" katika Biblia.

Kazi ya ziada
Andika tena kwa usahihi unayodhani sio kweli hapo juu.

16B Kazi ya ziada

Wa kwanza - Mungu; wa pili - Yesu; wa tatu - Malaika; wa nne - Mtu; wa Tano - Wanyama. Huu ni mpangilio wa muhimu sasa. Mpangilio wa muhimu ulikuwaje kabla ya Yesu kufa? (Waebrania 2:9 itakusaidia).

17A Ni kwa jinsi gani Yesu alikuwa kama Mungu, Baba yake?
17B Ni kwa jinsi gani Yesu alikuwa kama sisi?
17C Ni nini kilitokea Yesu alipojaribiwa jangwani?
17D Tunaweza kujifunza kitu gani kutokana na maisha aliyoishi Yesu?
17E Kazi ya ziada
Yesu katika Mahubiri ya Mlimani anasema jambo gani kuhusu:
(a) Talaka (Mathayo 5:32);
(b) Hazina (6:19-21);
(c) Kuhukumu wengine (7:1-5);
(d) Waalimu wa uongo (au manabii) (7:15-23).
17F Kazi ya ziada
Usome tena Mfano wa Mpanzi (Mathayo 13:1-8) na maelezo aliyotoa Yesu (Mathayo 13:18-23). Ikiwa mbegu ni Neno la Mungu, basi haya yafuatayo ni nini:
(a) Udongo wenye miamba;
(b) Miiba;
(c) Udongo mzuri?
Tunajifunza kitu gani kutoka kwenye mifano hii?

_____

18A Ni kwa sababu gani Yesu ilimbidi afe?
18B Kwa sababu zipi watu hawa walitaka kumuua Yesu:
(a) Viongozi wa Wayahudi;
(b) Pontio Pilato;
(c) Yuda Iskarioti?
18C Yesu alifanya kitu gani katika Bustani ya Getthemane?
18D Je! Yesu alitumia nguvu na kujaribu kuponyoka pale maaskari walipokuja kumkamata?
18E Je! Yesu alipenda kufa msalabani?
18F Andika kutoka 2 Wakorintho 5:15. Mstari huu unamaana gani?

18G Kazi ya ziada
Andika orodha ya sababu unazofikiri juu ya Zaburi 22 ya kwamba ulikuwa ni unabii wa kifo cha Yesu. (Linganisha Zaburi 22 na habari katika Injili juu ya kifo cha Yesu.)

_____

19A Ni nani aliye mfufua Yesu toka wafu?
19B Yesu yupo wapi kwa sasa?
19C Ni kwa jinsi gani atarudi duniani?
19D 1 Wakorintho 15:51 mstari unasema: "Hatuta lala sisi sote, bali tutabadilika".
(a) Hii maana yake nini?
(b) Huu unawahusu watu gani?
(c) Jambo hili litatokea lini?
19E Kazi ya ziada
Andika orodha ya watu waliomwona Yesu Kristo alipofufuka. (Luka 24 itakusaidia).

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

MASWALI KARATASI YA 4

Jaribu ujibu maswali kwa jinsi ulivyoelewa. Panaposema "kazi ya ziada" unaweza kujibu swali au ikiwa ni gumu unaweza kuacha. Tafadhali jaribu kujibu maswali yote mengine.

Kumbuka kuweka jina lako kwenye kila karatasi ya maswali na namba yako ya kuletewa masomo.

MASOMO 16-19

16A Kweli au sio kweli? Tenga haya yafuatayo yapi yaliyo sahihi na yasiyo sahihi:

(a) Mama yake Yesu alikuwa Mariamu.
(b) Baba yake Yesu aliitwa Yusufu.
(c) Yesu alikuwepo mbinguni kabla ya kuzaliwa.
(d) Mungu alijua tangu mwanzo ya kwamba angemtuma Yesu.
(e) Yesu alikuwa na umbo la mwanadamu kama sisi alipokuwepo duniani.
(f) Yesu ameitwa "Mungu Mwana" katika Biblia.

Kazi ya ziada
Andika tena kwa usahihi unayodhani sio kweli hapo juu.

16B Kazi ya ziada

Wa kwanza - Mungu; wa pili - Yesu; wa tatu - Malaika; wa nne - Mtu; wa Tano - Wanyama. Huu ni mpangilio wa muhimu sasa. Mpangilio wa muhimu ulikuwaje kabla ya Yesu kufa? (Waebrania 2:9 itakusaidia).

17A Ni kwa jinsi gani Yesu alikuwa kama Mungu, Baba yake?
17B Ni kwa jinsi gani Yesu alikuwa kama sisi?
17C Ni nini kilitokea Yesu alipojaribiwa jangwani?
17D Tunaweza kujifunza kitu gani kutokana na maisha aliyoishi Yesu?
17E Kazi ya ziada
Yesu katika Mahubiri ya Mlimani anasema jambo gani kuhusu:
(a) Talaka (Mathayo 5:32);
(b) Hazina (6:19-21);
(c) Kuhukumu wengine (7:1-5);
(d) Waalimu wa uongo (au manabii) (7:15-23).
17F Kazi ya ziada
Usome tena Mfano wa Mpanzi (Mathayo 13:1-8) na maelezo aliyotoa Yesu (Mathayo 13:18-23). Ikiwa mbegu ni Neno la Mungu, basi haya yafuatayo ni nini:
(a) Udongo wenye miamba;
(b) Miiba;
(c) Udongo mzuri?
Tunajifunza kitu gani kutoka kwenye mifano hii?

_____

18A Ni kwa sababu gani Yesu ilimbidi afe?
18B Kwa sababu zipi watu hawa walitaka kumuua Yesu:
(a) Viongozi wa Wayahudi;
(b) Pontio Pilato;
(c) Yuda Iskarioti?
18C Yesu alifanya kitu gani katika Bustani ya Getthemane?
18D Je! Yesu alitumia nguvu na kujaribu kuponyoka pale maaskari walipokuja kumkamata?
18E Je! Yesu alipenda kufa msalabani?
18F Andika kutoka 2 Wakorintho 5:15. Mstari huu unamaana gani?

18G Kazi ya ziada
Andika orodha ya sababu unazofikiri juu ya Zaburi 22 ya kwamba ulikuwa ni unabii wa kifo cha Yesu. (Linganisha Zaburi 22 na habari katika Injili juu ya kifo cha Yesu.)

_____

19A Ni nani aliye mfufua Yesu toka wafu?
19B Yesu yupo wapi kwa sasa?
19C Ni kwa jinsi gani atarudi duniani?
19D 1 Wakorintho 15:51 mstari unasema: "Hatuta lala sisi sote, bali tutabadilika".
(a) Hii maana yake nini?
(b) Huu unawahusu watu gani?
(c) Jambo hili litatokea lini?
19E Kazi ya ziada
Andika orodha ya watu waliomwona Yesu Kristo alipofufuka. (Luka 24 itakusaidia).

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England